

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: **"TUME"**  
DAR ES SALAAM  
Namba ya Simu:0738166703  
Fax: 255 - 022 – 2460117  
*e-mail:* [secretary@psc.go.tz](mailto:secretary@psc.go.tz);  
*Website:* [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)



TUME YA UTUMISHI WA UMMA,  
6 MATAA WA ALBERT LUTHULI,  
KITALU NAMBA 10,  
S.L.P. 9143,  
**DAR ES SALAAM.**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

---

Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kufanya Mkutano wa kazi na wadau wake tarehe 04 na 05 Juni, 2020 kupitia Miongozo inayotolewa na Tume ya Utumishi wa Umma ili kubainisha maeneo yenye changamoto katika utekelezaji wake.

Mkutano huo utaendeshwa kwa njia ya mtandao "video conference" kwa washiriki kuwa jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao - TaGLA na Dodoma katika ukumbi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI.

Bw. Bambumbile Mwakyanjala, Mkurugenzi wa Kitengo cha Miongozo, Uwezeshaji na Utafiti, Tume ya Utumishi wa Umma amesema jijini Dar es Salaam kuwa Tume ipo katika kuhuisha Miongozo ya Ajira na

Miongozo ya Nidhamu iliyotolewa mwaka 2009 kutokana na mabadiliko mbalimbali ya Sheria, pamoja na mabadiliko ya Kimiundo.

Miongoni mwa wadau wanaotarajia kushiriki ni kutoka katika Ofisi ya Rais-Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Kitengo cha Kazi-Mahakama Kuu; Ofisi ya Msajili wa HAZINA; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali; Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa mujibu wa ratiba ya mkutano kutakuwa na uwasilishwaji wa mada na majadiliano.

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Tume ya Utumishi wa Umma ni kutoa Miongozo na kufuatilia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu katika Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utumishi wa umma, Sura 298.

Imetolewa na:



Richard M. Cheyo  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Tume ya Utumishi wa Umma.

**DAR ES SALAAM**

03 Juni, 2020